**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# TAARIFA YA UKAGUZI NA UFUATILIAJI WA VYOMBO VYA WATUMIA MAJI (COWSOs) HALMASHAURI YA KALAMBO KATIKA MIRADI YA KAMAWE NA ULUMI KUANZIA TAREHE 24-25 JANUARI, 2017

Ofisi ya Mkuu wa Mkoa,
S.L.P 128,
**SUMBAWANGA.**

**JANUARI, 2017**

# TAARIFA YA UKAGUZI WA VYOMBO VYA WATUMIA MAJI (COWSOs) KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA KALAMBO

## Utangulizi:

Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo kupitia miradi ya maendelea ya sekta ya maji (WSDP) imetekeleza/inatekeleza miradi mbalimbali ya maji katika vijiji vyake. Ili miradi hiyo iwe endelevu Wizara ya Maji na Umwagiliaji ikaona ni vyema miradi inayokamilika kujengwa iendeshwe na wananchi wenyewe kwa kupitia vyombo huru vya watumia maji (COWSOs) zilivyoundwa kisheria na kupewa mafunzo na Halmashuri. COWSOs hizo zitafanya kazi kwa kufuata Katiba na kanununi zilizopangwa na wananchi kupitia mikutano mikuu ya vijiji.

Katika ukaguzi uliofanywa na Wataalamu kutoka Ofisi ya Mkuu wa Mkoa walifanikiwa kupitia na kukagua vyombo vya watumia maji (COWSOs) katika miradi miwili (2) ya Kamawe na Ulumi na kuona jinsi vinavyoendesha shughuli zake.
COWSOs hizozimetembelewa na taarifa ya kila COWSOs inaonekana kwenye jedwali lililoambatanishwa pamoja na taarifa hii.

## Dhumuni la Ukaguzi:

Ukaguzi huo umefanywa kwa madhumuni yafuatayo: -

i. Kuona taratibu za uudwaji wa COWSOs kama zimefuatwa
ii. Kuona namna COWSOs zinavyoendesha shughuli zake
iii. Kutoa ushauri katika changamoto mbalimbali zinazozikabili COWSOs zikiwemo namna bora ya uchangiaji wa huduma ya maji, Uandaaji wa taarifa za miradi na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla.

## Maoni ya jumla ya ukaguzi:

i. vyombo huru vya watumia maji (COWSOs) zilizotembelewa zipo katika hatua za kuandaa katiba na kuchagua wajumbe wa COWSOs
ii. vyombo huru vya watumia maji (COWSOs) zilizotembelewa zote hakuna iliyosajiliwa kisheria hivyo bado hazijaanza kufanya kazi kama vyombo vya watumia maji vilivyopo kutokana na sheria na taratibu
iii. Halmashauri kupitia Mhandisi wa maji ina kasi ndogo katika kusajili vyombo vya watumia maji na kupelekea miradi kukosa usimamizi mzuri

## Ushauri wa jumla wa ukaguzi:

i. Wataalamu wa Halmashauri wanashauriwa kufuata mtirirko mzima kama mwongozo unavyoelekeza katika uundwaji na usajili wa vyombo vya watumia maji (COWSOs) ikiwemo kuhusisha wananchi kupitia mikutano mikuu ya vijiji kwa zile COWSOs zinazoendelea kusajiliwa na zitakazosajiliwa

ii. Halmasahuri inatakiwa kuwa na mihtasari yote ya mikutano mikuu na mikutano mingine iliyofanywa wakati wa uundwaji wa vyombo vya watumia maji (COWSOs)

iii. Halmashauri inashauriwa kuwatumia Maafisa wa Maendeleo ya jamii katika uwamasishaji wakati wa uundaji wa vyombo vya watumia maji (COWSOs)

iv. Halmashauri inashauriwa kuharakisha uundaji na usajili wa vyombo vya watumia maji (COWSOs) kwa kufuata mwongozo ili miradi isimamiwe na kua endelevu

v. Halmashauri zinatakiwa kupata taarifa za hali ya mradi na taarifa ya mapato na matumizi kwa kila mwezi kutoka kwa viongozi wa COWSOs kupitia watendaji wa vijiji ili kuwa na ufuatiliaji wa karibu wa utendaji kazi

Washiriki:

Watumishi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa: -

1. Mhandisi wa Maji Shabani Kassim
2. Afisa Maendelea ya Jamii Aziza Kalyatila
3. Dereva Killian Mwambe

Mtumishi kutoka kwa Mkurugenzi wa Wilaya ya Kalambo: -

1. Msajili wa COWSOsEmmanuel Lema
2. Fundi sanifu Agatha Lyotto

| Jina la COWSO | Hali halisi ya COWSO | Ushauri/Maoni |
|---|---|---|
| Mradi wa maji Kamawe | • Chombo cha watumia maji (COWSO) bado hakijasajiliwa kwa sasa wanaendelea na taratibu za usajili.<br>• Wajumbe waliochaguliwa wapo 10 kati yao wanaume 6 na wanawake 4<br>• Mradi bado haujakabidhiwa kwa serikali ya kijiji na kabla ya kukabidhiwa mradi unatakiwa kufanyiwa marekebisho kwani maji yanatoka kidogo na hayatoki vituo vyote kutokana na solar kupungua nguvu pindi jua linapokata<br><br>Mikakati ya utunzaji wa vyanzo<br>Kijiji kinaonyesha hakina mikakati yeyote ya utunzaji wa chanzo cha maji kwani wamezidiwa na wananchi wanaolima katika vijiji vya Ngoma, Ziangoma na Kankoa ambapo mto ndipo unapotokea | • Halshauri inashauriwa hadi kufikia tarehe 01/02/2017 COWSO iwe imeshasajiliwa na baadae kupatiwa mafunzo kwa wajumbe ili wajumbe waliochaguliwa waaanze kufanya kazi<br>• Halmashauri kupitia mkandarasi ifanye marekebisho ya solar ili pampu iweze kusukuma maji wakati wote<br>• Halmashauri ifuatilie watu waliovamia chanzo cha maji kinachotumika na kijiji cha kamawe kwani kinaharibiwa na watu wa vijiji vya Ngoma, Ziangoma na Kankoa<br>• Mchoro wa “As Built drawing” uchorwe kuwezesha kufuatilia kwa uraisi wakati hitirafu inapotokea |
| Mradi wa maji Ulumi | • Chombo cha watumia maji (COWSO) kimeundwa bila kufuata taratibu zote kama mwongozo unavyoelekeza<br>• COWSO iliyopendekezwa kuundwa ina wajumbe 20 ambao ni wengi sana | • Halmashauri inashauriwa kuunda upya chombo cha watumaji maji (COWSO) katika mradi wa Ulumi kwa kufuata taratibu zote kama mwongozo unavyoelekeza kwa muda usiozidi wiki mbili (2) |

| | | |
|---|---|---|
| | | • COWSO itakayounda izingatie usawa wa kijinsia |

PICHA

| | |
|---|---|
|  |  |
| Baadhi ya wajumbe teule wa COWSO-Kamawe | Kituo cha maji cha jumuiya - Kamawe |